# Kigamboni 2022

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni

Toleo Namba 01, Julai-Septemba kwa Mwaka wa fedha 2022/2023

JARIDA LA MKUSANYIKO WA HABARI MBALIMBALI

# Hospitali ya Wilaya Kigamboni yanufaika na Msaada wa vifaa tiba kutoka Ujerumani uliotolewa kwa Hospitali za Wilaya Dar es Salaam .



Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe.Amos Makalla akikabidhi vitanda kwa viongozi wa Wilaya ya Kigamboni walipokuwa wakipokea vitanda hivyo kwenye hospitali ya Wilaya, kulia ni Mbunge wa Kigamboni Mhe.Faustine Ndungulile, Meya wa Manispaa ya Kigamboni Mhe. Ernest Mafimbo na kulia ni Katibu Tawala Mkoa Ndg.Hassan Rungwe na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa.

# Hospitali ya Wilaya Kigamboni yanufaika na Msaada wa vifaa tiba kutoka Ujerumani kwa Hospitali za Wilaya Dar es Salaam .

Tarehe 22/7/2022 Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni ilipokea vifaa tiba (vitanda 108 na kabati zake 38 pamoja na vyuma 161 vya kunin'ginizia miguu na dripu) mara baada ya uzinduzi wa vifaa hivyo uliofanywa na Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mh.Amos Makalla ambae alikuwa ni mgeni rasmi aliezindua vifaa hivyo na kukabidhi kwa Wilaya 5 za Mkoa wa Dar es salaam.

Akiongea katika uzinduzi huo Mkuu wa mkoa aliwashukuru wadau hao kutoka Hamburg Germany ambao Wana ushirikiano na Tanzania wa muda mrefu tangu mwaka 2007. Pamoja na hayo alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kudumisha mahusiano na nchi za nje ambapo katika kipindi chake mahusiano yameimarika na kuinufaisha nchi yetu.Pia aliipongeza Manispaa ya Kigamboni kwa jinsi inavyokua kwa Kasi kutokana na kazi nzuri inayoendelea kufanywa.

Aidha alisema kuwa msaada huo ni wa awamu ya pili ambapo kuna container zingine zitakuja zitakazoleta vifaa tiba vingine vitakavyosambazwa pia kwenye vituo vya afya vinavyoendelea kujengwa kwenye Wilaya za Dar es Salaam.

Mbunge wa Kigamboni Mh.Ndugulile akiongea katika hafla hiyo alimshukuru Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoinyanyua kigamboni



Picha za Vitanda vilivyokabidhiwa kwaajili ya kuboresha hali ya utoaji wa huduma kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni.

kimaendeleo ikiwepo kuipatia pesa mil 420 za UVICO ,mkopo wa Bil.1.5 kwa Manispaa kwa ajili ya kuendelea kuipanga Kigamboni na sekta ya afya ununuzi wa X-ray katika Hospitali ya Wilaya ambayo ilikuwa kero kubwa. Licha ya hayo alimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa utendaji wake na usimamizi na kuifanya Wilaya kwenda kwa Kasi katika maendeleo katika Nyanja mbalimbali.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almas Nyangasa Kigamboni aliwashukuru wadau hao kwa msaada huo kwani utasaidia kutatua upungufu uliokuwepo, Aidha alimshukuru Rais wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuifungua nchi na kupelekea kuongezeka kwa mahusiano baina ya nchi yetu na nchi za nje. Pia alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam kwa jinsi ambavyo amekuwa akitupia jicho katika kila sekta kuhakikisha Dar es salaam inafanya vizuri.

Akiongea Meya Manispaa ya Kigamboni Mh Ernest Mafimbo alimshukuru kwa kupatikana vifaa hivyo kwani vinaenda kutatua changamoto iliyokuwepo ya uhaba wa vitanda.

Wilaya zingine zilizonufaika ni Ilala, Kinondoni, Ubungo na Temeke

# KIGAMBONI 2022

## Ijue Miradi ya Elimu Msingi iliyokamilika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na fedha za mapato ya ndani.



Wanafunzi wa Darasa la Sita Shule ya Msingi Raha leo wakiwa kwenye masomo ya makundi kwenye moja ya darasa lililojengwa kwa mapato ya ndani.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imeendelea kutekeleza maagizo ya Serikali ya kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo kwa Mwaka wa fedha wa 2021/2022 kupitia mapato yake ya ndani imeweza kukamilisha miradi kadhaa ya Elimu Msingi na miradi mingine ikiendelea kutekelezwa.

Katika Kata ya Pembamnazi Manispaa imeweza kujenga na kukamilisha ujenzi wa madarasa 2 katika Shule ya msingi Buyuni ambapo hadi kufikia Juni 2022 mradi huo ulikuwa umekamikika na kuanza kutumika na kiasi cha shilingi mil.40 zilitumika kwenye ujenzi , Pia kiasi cha mil.54,720,000 zimetumika kujenga madarasa 3 katika Shule ya Msingi Kichangani na madawati 60 yametengenezwa.

Aidha katika kata ya Kigamboni Manispaa imemalizia ujenzi wa madarasa 2 na ujenzi wa darasa 1 Shule ya Msingi Rahaleo pamoja na utengenezaji wa madawati 50 ambapo Jumla ya shilingi mil.40 zimetumika.

Kata nyingine ni ya Kimbiji ambapo huko limejengwa darasa 1 na madawati 25 yametengenezwa, mradi umekamilika na kuanza kutumika. Jumla ya shilingi mil.20 zimetumika kukamilisha mradi.




Watoto wa Darasa la kwanza Shule ya Msingi Kisiwani wakiwa kwenye moja ya darasa lililojengwa kwa fedha ya mapato ya ndani.

# Ijue Miradi ya Elimu Msingi iliyokamilika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na fedha za mapato ya ndani.

Kwa upande wa Kata ya Mjimwema Shule ya Msingi Kibugumo umaliziaji wa ujenzi wa madarasa 2 umefanyika na madawati 50 yametengenezwa na kuanza kutumika.Gharama iliyotumika ni mil.27,413,900.

Kata ya Vijibweni ujenzi wa umaliziaji madarasa 2 umefanyika katika shule ya Msingi Kisiwani,Jumla ya mil.30,143,500 zimetumika na madawati 50 yametengenezwa ili kuboresha mahali pa kufundishia wanafunzi.



Madarasa mawili yaliyojengwa kwa fedha za mapato ya ndani Shule ya Msingi Kibugumo ambayo tayari yanatumika.

Kata ya Kisarawe II Shule ya Msingi Chekeni Mwasonga, Manispaa ilitoa kiasi cha shilingi mil.44,024,000 kwa ajili ya umaliziaji wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo fedha zingine zilitoka serikali kuu kiasi cha shilingi mil.80.

Jumla ya shilingi millioni 48 zimetumika kutengeneza Madawati 505 katika Kata ya Kibada ambapo Shule zifuatazo zimenufaika na madawati hayo, Shule ya Msingi Darajani,Ungindoni,Kibugumo,Mbutu, Vijibweni,Vumilia ukooni,Gomvu,Kimbiji,Kijaka,Kisarawe II,Mizimbini,Juhudi na Kibada.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kibugumo Ndg Lucas alisema anamshukuru Mkurugenzi kwa kuboresha miundombinu ya madarasa na madawati, kwa kujenga madarasa hayo mawili yaliyolenga la kupunguza ule uhaba wa maradasa waliyokuwa nayo hususani katika kipindi hiki cha Elimu bila Malipo, ambapo imeongeza kwa kiasi kikubwa ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Msingi kila mwaka tofauti na miaka ya nyuma.

Ameongeza kuwa Shule yake inawafunzi 2064 hivyo kuongezewa miundombinu ya madarasa na Madawati ni hatua kubwa kulingana na uhitaji walionao na kumuomba Mkurugenzi aendelee na mpango huo mzuri.

Shakira Bakari Nyumba ni mwanafunzi wa Darasa la Sita Shule ya Msingi Kibugumo anasema kuwa anashukuru kwa sasa msongamano wa wanafunzi umekuwa mdogo na wanaweza kusoma kwa nafasi tofauti na awali kabla ya madarasa hayo kujajengwa na kuwekwa madawati.



Baadhi ya Madawati yaliyotengenezwa kwa fedha za mapato ya ndani

# Wenyeviti wa Serikali za Mitaa watakiwa kuimarisha ulinzi shirikishi



Baadhi ya wenyeviti wa Mitaa wakisikiliza kwa makini maelekezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya ulinzi na usalama Wilaya Mheshimiwa Fatma Almas Nyangasa



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mheshimiwa Fatma Almas Nyangasa akizungumza na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kuhusu sula la ulinzi na usalama kwenye maeneo yao.

Mwenyekiti wa kamati ya Ulinzi na usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mheshimiwa Fatma Almas Nyangasa amewaelekeza Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ambao pia ni wenyeviti wa kamati za ulinzi katika ngazi ya Mitaa yao kuhakikisha ulinzi shirikishi unafanyika kikamilifu sambamba na utoaji taarifa ya hali ya usalama katika maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya aliyazungumza hayo Katika kikao kazi Maalum na wenyeviti wa Serikali za Mitaa kilichofanyika kwenye ukumbi wa mkuu wa Wilaya, Nyangasa aliwatahadharisha vijana kutojihusisha na vitendo vya uhalifu kwani tayari Jeshi la polisi Wilaya ya Kigamboni limeanza oparesheni Maalum ya Kata kwa Kata na kuwataka wazazi kuwaonya vijana wao kutokujihusisha na vitendo vya kihalifu.

Sambamba na hila Mhe.Nyangasa aliwataka Wananchi kutoa taarifa haraka kwa jeshi la polisi juu ya mtu, kikundi au mazingira yoyote yenye mashaka ili zifanyiwe kazi kukabiliana na vitendo vya uhalifu kwa ujumla.

Naye Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kigamboni OCD Thobias Walelo alisema timu yake iko timamu kuhakikisha usalama Kigamboni unaendelea kuimarika, huku akiwataka wananchi kutoa ushirikiano katika upatikanaji taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wenyeviti wa serikali za mitaa yote pamoja na Watendaji wa Kata zote za Manispaa ya Kigamboni.

# Wazazi na Walezi watakiwa kuwa mabalozi kwenye jamii chanjo ya polio.

Hayo yalijiri katika Hospitali ya Vijibweni ambapo Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almas Nyangasa aliwataka walezi na wazazi walioshiriki katika Uzinduzi huo kwenda kuwa mabalozi katika jamii na kuwaelimisha wengine juu ya umuhimu wa chanjo ya Polio kwa ajili ya afya ya watoto.

Mkuu wa Wilaya alisema Serikali imewekeza katika afya na imeendelea kuboresha sekta ya afya kwa kuweka nguvu katika kuwezesha chanjo hii hivyo wana Kigamboni wanaendelea kumshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika hilo.

Aidha aliwataka walezi na wazazi kudumisha usafi katika majumba yao kwani uchafu ni chanzo kikubwa cha ugonjwa huu wa polio ambao huambukiza na kupelekea mtoto kupooza.

Kuhusu utekelezaji wa zoezi hilo la chanjo Mhe. Nyangasa alisema tayari kuna timu ya watu 59 ambao wapo katika makundi ya watu watatu watatu ambao watapita nyumba kwa nyumba kwa ajili ya kutoa chanjo hiyo hivyo, wazazi na walezi wawatoe watoto wao waweze kupata chanjo,sambamba na hilo aliwataka wasisite kuuliza maswali pale wanapotaka kufafanuliwa jambo lolote kwani kila mmoja anawajibika kwa nafasi yake katika kufanikisha utolewaji wa chanjo hiyo.

“Hili ni Jambo letu wote tuhakikishe watoto wamepata chanjo na kufanya Taifa kuwa na kizazi salama.”alisema Mhe.Nyangasa.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mh.Fatma Almas Nyangasa akimshika mtoto kwaajili ya kupewa chanjo ya Polio huku akiwahamasisha wazazi na walezi kuwa mabalozi kwenye jamii zao ili kuwezesha watoto wote kupata chanjo hiyo.

Katika zoezi lililopita Wilaya ya kigamboni ilifanikiwa kuvuka lengo kwa kuchanja watoto 37000 tofauti na lengo walilojiwekea la watoto 30000. Shime wazazi tuwatoe watoto wapate chanjo kuepuka madhara ya polio.



Baadhi ya wazazi na walezi waliofika kuwapatia watoto wao chanjo ya polio kwa lengo la kumkinga mtoto na maradhi ya kupooza.

# Usimikaji mashine ya X-Ray katika kituo cha afya Kimbiji kuboresha huduma ya afya



Mashine ya X-Ray iliyosimikwa kwa lengo la kuboresha utoaji wa afya Kimbiji.

Mkuu wa Wilaya Mhe.Fatma Almas Nyangasa aliyasema hayo tarehe 31/9/2022 alipofanya ziara ya kukagua usimikaji wa mashine ya X-Ray katika kituo cha afya Kimbiji.

Akiongea mara baada ya ukaguzi huo Mhe.Nyangasa alisema mashine walikuwa wakifata huduma za x-ray umbali wa kilometa 20 lakini sasa huduma hiyo imesogezwa karibu na itasaidia wananchi wa kata hiyo na Kata jirani ya Pembamnazi.

Akiongelea jitihada za serikali alisema anamshukuru Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada za kuboresha huduma za afya Kigamboni na hata kupata shillings mil.365 katika bajeti ya 2022/2023 kwa ajili ya miundo mbinu ya afya,vifaa tiba .

Aidha alisema huduma ya X-Ray itaanza hivi karibuni.

# Manispaa ya Kigamboni yapaa ukusanyaji mapato,TAMISEMI yapongeza

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imeshika nafasi ya pili kwa Halmashauri za Manispaa zote nchini kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kigezo cha asilimia ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serkali za Mitaa, Innocent Bashungwa (Mb) kuhusu Mapato na Matumizi ya Mapato ya Halmashauri zote 184 nchini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 aliyoisoma jijini Dar es Salaam tarehe 02 Agosti 2022, imeainisha kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa kipindi cha mwaka husika ilipanga kukusanya shilingi bilioni 9,106,000,000 kupitia mapato yake ya ndani ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2022 ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 10,761,334,792 sawa na asilimia 118.

Uchambuzi unaonesha kwamba, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ni miongoni mwa Manispaa iliyokusanya mapato yake kwa zaidi ya asilimia 100.

Pongezi nyingi Sana ziwaendee Mkuu wa Wilaya ya kigamboni Mh.Fatma Almas Nyangasa,Meya wa Manispaa Mh.Ernest Mafimbo kwa usimamizi mzuri.Aidha Mkurugenzi wa Manispaa Ndg. Erasto Kiwale kwa utekekezaji wenye ufanisi pamoja na timu yake ya menejimenti.



# KIGAMBONI 2022

## Timu ya Menejimenti ya Manispaa Kigamboni wakagua miradi 3 yenye lengo la kuongeza mapato ili kuona hatua za utekelezaji zinazoendelea.

Ziara hiyo ilifanyika tarehe 6/9/2022 ambapo timu ya Menejimenti ya Manispaa ya Kigamboni walikagua miradi yenye lengo ya kuiongezea Manispaa mapato itakapokamilika.

Miradi hiyo ni ujenzi wa Soko la mazao linalojengwa katika kata ya Somangila ambapo mpaka kukamilika kwake jumla ya Tshs.milioni 100 zitatumika, mpaka sasa Manispaa imeshatoa mil.50 za mapato ya ndani na tayari kiasi kilichobaki kimeingizwa katika bajeti ya 2022/2023.Litakapokamilika soko hili litaiongezea halmashauri mapato kupitia ushuru utakaokuwa unalipwa na wafanyabiashara watakaokuwa wanatumia soko hili, pamoja na kusogeza huduma Kwa wananchi wa eneo hili ambao hawana huduma ya Soko.

Mradi mwingine uliokaguliwa ni mradi wa ujenzi wa Machinjio ambapo mradi huu Hadi Kwisha kwake utagharimu Tshs.mil 180 chanzo cha fedha kutoka mapato ya ndani, katika awamu ya Kwanza ya utekelezaji tayari millions 80 zimeshatolewa .Mradi huu utakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 20 mpaka 30 kwa siku.

Pamoja na miradi hiyo timu ya menejimenti pia iliweza kukagua mradi wa ujenzi wa sehemu ya abiria kupandia daladala (shade) katika stendi inayotarajiwa kujengwa katika eneo la NAFCO



Jengo la soko la mazao linalojengwa Kata ya Somangila ambapo hadi kukamilika kwake litagharimu milioni 100 na kuwezesha wananchi kuwa na soko la uhakika pia kuingizia mapato Manispaa.

ambapo kutokana na mahusiano mazuri ya Manispaa na wadau wa Kigamboni Kampuni ya Lake Cement wamejitolea kujenga sehemu hiyo kwa nia ya kurudisha huduma kwa jamii (CSR) na kuonyesha mchango wao kama sehemu ya kuwajibika kwa jamii inayowazunguka.

Akiongea kiongozi wa timu hiyo ya ukaguzi wa miradi ambaye ni Kaimu Mchumi kwa niaba ya Mkurugenzi Bi.Eutropia Mlela alisema wameridhishwa na maendeleo ya miradi waliyokagua kwa kuwa imekuwa na maendeleo mazuri tofauti na walipokagua mara ya mwisho.

Walimshukuru Mkurugenzi na wasimamizi wa Idara husika kwa ushirikiano katika utekelezaji wa miradi hiyo yenye lengo la kuongeza tija katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Manispaa,lakini pia kuongeza huduma bora Kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Tawala CCM.

# Bilioni 1.2 kunufaisha Sekta ya Elimu Sekondari kwa mwaka wa fedha 2022/2023



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kidete wakiwa kwenye moja ya Darasa lililojengwa kwa fedha za Uviko wakijiandaa kuanza masomo.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1,225,251,681.56 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa lengo la kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya elimu upande wa Sekondari.

Fedha hizo zitaenda kutekeleza miradi mbalimbali ambayo ni ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya Utawala,ujenzi wa shule mpya ya sekondari,ununuzi wa madawati,ukarabati wa madarasa kwa yale yanayohitaji ukarabati na umaliziaji wa miundombinu.

Kwa upande wa ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya Utawala kata ya Kisarawe II Shule zitakazonufaika ni Shule ya sekondari Kisarawe II na shule ya sekondari Nguva kwa kukamilishiwa majengo hayo ambapo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kutatua kero ya waalimu kukosa sehemu sahihi na yenye usalama katika utekelezaji wa shughuli zao wawapo shuleni .

Aidha utafanyika ukamilishaji wa miundombinu ya vyoo, uzio na madarasa katika Shule ya Sekondari Paul Makonda.

Ili kutatua kero za kubanana kwa wanafunzi Manispaa pia imepanga kutumia fedha hizo kwa ajili ya ununuzi wa madawati 600 kwa Shule za Sekondari .

Pamoja na hayo ili kutekeleza takwa la kiafya Manispaa kwa mwaka huu wa fedha itaboresha mazingira ya vyoo kwa kujenga matundu 5 ya vyoo vya waalimu katika Shule ya Sekondari Kibada na matundu 5 katika shule ya Sekondari Mizimbini.

Kama tunavyojua Elimu ya sayansi na teknolojia imeshika kasi katika Karne hii, ili kuendana na Kasi hii Manispaa imeamua kuhakikisha inafanya ukamilishaji wa maabara za shule katika Kata zote ili Kurahisisha masomo haya ya sayansi kufundishwa kwa vitendo na kuleta ufanisi zaidi.

Aidha Manispaa pia imejipanga kukarabati jumla ya madarasa 32 ambapo kwa kila shule yatakarabatiwa madarasa manne (4) kwenye shule za Sekondari za Tungi, Minazini, Vijibweni, Pembamnazi,Kisarawe II,Aboud Jumbe,Nguva na Kidete.

Aidha fedha hizo pia zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Mkoa wa Dar es Salaam ambayo itakuwa kwenye Kata ya Somangila.

Manispaa inatarajia pia kumalizia wa ujenzi wa Maktaba,chumba cha ICT na vyoo vya walimu katika shule Shikizi ya Tundwi Songani iliyojengwa kutokana na mradi wa SEQUIP.

Afisa elimu Sekondari Bi.Restituta Mtaita alisema hadi kukamilika kwa miradi hii Manispaa itaweza kutatua kwa kiasi kikubwa miundombinu inayotegemewa katika kukuza ufundishaji na ufundishwaji hali itakayoboresha utoaji wa elimu bora.

# KIGAMBONI 2022

## Wazee 3518 Kigamboni wanufaika na vitambulisho vya msamaha wa malipo ya matibabu,watakiwa kuyatumia vizuri mabaraza ya wazee.

Rai hiyo ilitolewa katika hafla ya maadhimisho ya siku ya Wazee duniani ambapo Manispaa ya Kigamboni iliadhimisha katika viwanja vya Mjimwema tarehe 5/10/2022.

Akiongea Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almasi Nyangasa ambae pia alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliwapongeza wazee kwa jinsi walivyotoa ushirikiano kwa uongozi Wilaya kwa kujitokeza pale walipoitwa na kusisitiza kuwa Serikali inawatambua na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Samia Suluhu anawathamini na anatambua mchango wao katika Taifa na hivyo, kuwaasa kuyatumia vizuri mabaraza ya wazee kwa kushirikiana na watendaji katika Kata zao.

Akiongelea kuhusu maombi mbalimbali (naomba ombi walau moja au mawili waliyoyatoa) yaliyoainishwa katika risala yao



Baadhi ya Wazee walioshiriki kwenye maadhimisho ya siku ya Wazee

DC Nyangasa alisema kuwa ameyachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi Aidha alimshukuru Mkurugenzi Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Ndg. Erasto Kiwale kwa utekelezaji wa maagizo mbalimbali ambayo amekuwa akimpa kuhusiana na maswala ya wazee.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg. Erasto Kiwale alieleza kwa jinsi Manispaa inavyotekeleza maagizo ya Serikali kuhusiana na maswali ya wazee likiwepo suala la kutoa vitambulisho vya msamaha wa malipo ya matibabu kwa wazee ambapo wazee 3518 wameshapatiwa vitambulisho hivyo.

Aidha alisema Manispaa imekuwa ikitoa elimu ya Chanjo ya COVID -19 kwa wazee ambapo wazee 2228 walipata elimu hiyo,pamoja na hilo Manispaa imesimamia uundaji wa mabaraza 77 kwa wazee kuanzia ngazi ya Wilaya, Kata na mtaa, pia Manispaa imeendelea kutoa elimu ya saikolojia kwa wazee na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilifanikiwa kutumia mil.7.4 kuwakatia bima wazee kwa ajili ya unafuu wa matibabu.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa(kushoto) akiandika baadhi ya changamoto zinazowasilishwa na wazee na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg.Erasto Kiwale akifuatilia hoja zinazotolewa.

# Madiwani kigamboni waielekeza menejimenti kuweka alama maeneo yote hatarishi na kuhamasisha kwa juhudi udhibiti wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi



Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg.Erasto Kiwale akipokea maelekezo ya Baraza kwa utekelezaji.

Baraza la Madiwani limemuagiza Mkurugenzi wa Manispaaya Kigamboni pamoja na timu ya mejimenti kuweka alama ya katazo ya uendeelezaji kwenye maeneo yote hatarishi, kuandaa michoro pamoja na kuandika andiko litakalosaidia kutafuta ufadhili utakaosaidia kujenga mkondo maalumu wenye nguvu ya kukusanya maji kuelekea baharini, ili kunusuru Makazi ya watu yanayoathirika na maji yanayotawanyika kutoka kwenye bwawa la Boko linalochukua maji kuoka maeneo mbalimbali kuelekeza baharini.

Akizungumza wakati wa Mkutano wa Baraza lililofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa Meya wa Kigamboni Mhe. Ernest Mafimbo alisema, Mtaa wa Magogoni ni eneo ambalo linaathirika kwa asilimia kubwa kwani miundombinu ya kumwaga maji kutokea Daraja la Nyerere kueelekea baharini yanapita kwenye mkondo huo ambao unapita kwenye bwawa la boko lililopo kwenye mtaa huo hivyo, kipindi cha mvua nyumba nyingi zinazungukwa na maji kupelekea athari za watu na makazi kutokana na utambalale wa mkondo huo.

Akizungumzia upande wa udhibiti wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi Meya alisema wamewaagiza wataalamu kurejesha utaratibu wa kupanga ratiba ya kuonesha sinema za uelimishaji juu ya ukimwi, kuona athari na kupata tahadhari ya kujiepusha kwani janga hili bado lipo kwa kuangalia takwimu za kwenye vituo vyetu vya afya.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kimbiji Mhe. Sanya Bunaya alisema kuwa wananchi wamejishahu na kutumia njia ambazo sio sahihi za kujikinga na maambukizi ya virusi vya ukimwi na kuacha kufuata maelekekezo ya wataalamu ya namna bora ya kujikinga na maambukizi hali inayopelekea ongezeko la maambukizi hayo

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kigamboni Mhe. Yahaya Shabani alisema anashukuru kushiriki kikao cha Baraza la Madiwani kwa mara ya kwanza tangu kuchaguliwa kwake ameona kigamboni inaendelea kukua kwa kasi hivyo kwa kusikiliza hoja za wataalamu na Madiwani anaamini itaendelea kufunguka zaidi kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg.Erasto Kiwale alisema amepokea maelekezo yote na atashirikiana na timu ya menejimenti pamoja na wadau wengine ili kuhakikisha yanafanyiwa kazi kama yalivyoelekezwa kwa weredi.

Baraza la madiwani limejadiri pia taarifa za maendeleo za kamati mbalimbali ikiwa ni utaratibu wa kila mwisho wa robo ya kwanza ya kukamilika.



Baadhi ya Madiwani wakifatilia uwasilishwaji wa majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa wakati wa Baraza kutoka kwa Mkurugenzi.

# KIGAMBONI 2022

## HABARI KATIKA PICHA





Muonekano wa Beach ya Kidete iliyopo Gezaulole eneo la Kidete inayotengenezwa na Manispaa ya Kigamboni ili kuwezesha wananchi kuweza kupumzika kwenye fukwe ambapo hadi sasa miundombinu ya vyoo, maeneo ya kupumzikia watu inaendelea kuwekwa













Mwananchi Hamasika kulipia Ada, Tozo, Vibali na Ushuru wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ili kuwezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo upande wa elimu, afya na mikopo ya asilimia 10 isiyokuwa na riba na ujenzi wa miundombinu kwa kutumia Mapato ya ndani


### Mwandishi na Mhariri
Mariam Makombe

### Mtayarishaji
Alda Phestor Sadango

### Waharii wengine
Joseph Semkiwa
Rose Mligo
Honorata Minde


### Tupate kupitia mitandao ya jamii ya
kigambonimanispaa KGMC TV

DIRA(VISION)

Kuwa na jamii iliyoelimika na yenye maisha bora kufikia 2025

DHAMIRA( MISSION)

Kutoa huduma bora za kijamiii na kiuchumi kwa kutumia kiufasaha rasilimali zilizopo na utawala bora kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi

**LIMEANDALIWA NA : KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI KIGAMBONI.**



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**
**S.L.P 36009, DAR ES SALAAM**
**www.kigambonimc.go.tz**